



SWAHILI A1 – STANDARD LEVEL – PAPER 1
SOUAHÉLI A1 – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1
SWAHILI A1 – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1

Monday 19 May 2003 (morning)

Lundi 19 mai 2003 (matin)

Lunes 19 de mayo de 2003 (mañana)

1 hour 30 minutes / 1 heure 30 minutes / 1 hora 30 minutos

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Write a commentary on one passage only. It is not compulsory for you to respond directly to the guiding questions provided. However, you may use them if you wish.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- Ne pas ouvrir cette épreuve avant d'y être autorisé.
- Rédiger un commentaire sur un seul des passages. Le commentaire ne doit pas nécessairement répondre aux questions d'orientation fournies. Vous pouvez toutefois les utiliser si vous le désirez.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Escriba un comentario sobre un solo fragmento. No es obligatorio responder directamente a las preguntas que se ofrecen a modo de guía. Sin embargo, puede usarlas si lo desea.

Kifafanue kimoja kati ya vifungu vifwatavyo:

1. (a)

	Ungamuona kuhani Ang'aka na kujighani Jitulize kwa makini Kusema ni kwetu sote	anena hamezi mate malumbi ashinda wote akili asikuchote mawazo ni kwa wachache
5	Urembo wa binadamu Usikutiye hamumu Twaa kidogo sehemu Kusema ni kwetu sote	na uzawa pande zote ukamba hanayo tete mengine mwache agute mawazo ni kwa wachache
10	Hata vitisho na nguvu Maguvu si saidivu Ukaechi kwa utuvu Kusema ni kwetu sote	kichwani mwako yafute yapishe njia yapite na moyo usikutute mawazo ni ya wachache
15	Mathali mtu tajiri Iwa ni mwenye nadhari Kwenda anayo dosari Kusema ni kwetu sote	kajaaza kote kote wenende kisha usite dhibiti asikuvute mawazo ni ya wachache
20	Uaminifu na vyeo Wangapi wachafuao Malumbanaji ni chuo Kusema ni kwetu sote	tumbo yasikirekete na hadhi wazifumbate pekee tulikamate mawazo ni kwa wachache

Kutoka *Malenga wa Mrima* na Mwinyihatibu Mohamed (1986)

- Mshairi anawasilisha ujumbe gani katika shairi hili?
- Vipi mshairi amefanikiwa au kutofanikiwa katika kuwasilisha ujumbe wake? Na vipi anatumia ‘chuku’ na ‘vitia-chumvi’ katika kuonyesha watu wenye vyeo na walio madarakani ni vigeugeu na hawana uthabiti.
- Toa maoni yako kuhusiana na ujumbe anaouwasilisha.

1. (b)

Vitu nya duka la Bugebuge sasa vilikuwa vinahesabika. Sehemu nyingi za duka sasa zilikuwa na mapengo. Sehemu ambazo zamani zilishamiri kwa vitu nya aina nyingi sasa zilikuwa tupu kama kinywa cha kibogoyo ambaye katu hakufikiria kuota meno tena. Kama Bugebuge angeamua kufanya “stock checking” angetumia dakika ishirini tu. Unga ulikuwa mwingi, maharagwe, choroko, mchele na mafuta ya taa, mafuta ya uto na vitu vingine nya aina hiyo. Vitu nya makopomakopo na aina kama hiyo vilikuwa vichache mno. Labda utajumlisha pia vibatari vingi vilivyoning’inizwa kwa kamba toka mti mmojawapo wa darini. Pia na kata za mabati za ukubwa na miundo mbalimbali.

10 Vipande nya fenesi ambavyo vilikuwa kwenye bao mbele ya duka havikukawia kwisha, hasa vilenunuliwa na watoto wa shule. Lakini duka gani laweza kudumishwa kwa kuuza vipande nya fenesi, kipande kimoja shilingi, hata kama vinauzwa vipande mia kwa siku? Pengine lingekuwa jambo muafaka kama vipande vile vingeingizwa ndani ya duka kuziba yale mapengo kwenye yale marafu matupu. Hii ingempunguzia Bugebuge au mwingine yejote yule kazi ya kufukuza nzi bila ya kusumbuka sana. Vipande nya papa; vile virefu kama miche ya sabuni viliegeshwa kwenye marafu. Ama kwa hakika lilikuwa duka la aina yake.

20 Ukiruka upande wa pili wa barabara mambo yalikuwa tofauti. Duka la Chambo lilikuwa likisitawi vizuri mno. Lilijaa watu wakati wote. Kitu chochote ambacho ungekipata kwenye maduka ya Tanga, Korogwe au Muheza kilipatikana pale. Kilichogomba kwa mnunuzi ni kuwa na pesa tu. Yeye hakukubali kukopesha kama ilivyokuwa kwa Bugebuge.

25 Pia ukihesabu hatua kama ishirini nyuma ya duka la Chambo palijengwa banda ambalo wenyeji hawakujua ni la kazi gani mpaka siku moja lori la Chambo lilipofika kutoka Tanga.

30 Lori ambalo mngurumo wake ulisikika toka mbali ulifanya kuwasili kwake kuvutie hisia za kila mtazamaji. Ndani ya lori kulikuwa na mashine moja kubwa ambayo ilisababisha utafiti mwingi mionganoni mwa waliokuwepo. Lori lilikwenda kusimama kwenye lile banda lililomalizika karibuni. Mashine iliyokuwemo ndani ya lori ilikuwa ya kusagia nafaka.

Kutoka *Funke Bugebuge* na Edwin Semzaba (1999)

- Katika kuandika kifungu hiki mwandishi alikuwa na dhamira gani?
- Ielezee taathira ya mbinu ya ulinganishi katika kifungu hiki.
- Kwa kutumia msingi wa maelezo haya elezea migogoro inayoweza kuzuka baina ya wahusika Bugebuge na Chambo.
- Toa maoni yako kuhusu usimulizi na lugha aliyotumia mwandishi katika kifungu hiki.